# MSALABA NI ISHARA YA WOKOVU WETU

**D. W. MINJA**




(a) Yule nyoka, wa zamani, juu ya mti walimtazama wakapona.
(b) Sisi leo, tumtazame, Bwana Yesu juu ya msalaba tuokoke.

(a) Msalaba, ni alama, ya upendo, utii na unyenyekevu
(b) Bwana Yesu, ni mfano, wa fadhila kwa kifo cha- msalaba

(a) Msalaba, ni maisha, ya uchaji kwa Mungu na kwa wanadamu.
(b) Ni mawazo, ni maneno, na matendo yasiyopingana na Mungu.

(a) Msalaba, ni sadaka, ya maisha kwa Mungu na jirani zetu.
(b) Ni kuacha ya Dunia, kwa ajili ya utukufu wa mbinguni.

(a) Bwana Yesu, alisema, Mfuasi lazima kwanza ajikane
(b) Ajitwike, msalaba, amfuate popote pale aendapo.